

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
29 Oktoba, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anatarajia kuondoka nchini leo tarehe 29 Oktoba, 2024 kuelekea Des Moines, Iowa, nchini Marekani kuhudhuria Mjadala wa Kimataifa wa Norman E. Borlaug ulioandaliwa na Taasisi ya World Food Prize Foundation ya nchini humo.

Mjadala wa Kimataifa wa Norman E. Borlaug hufanyika kila mwaka na kuhudhuriwa na viongozi, wataalamu, watu mashuhuri, watunga sera, hususan za kilimo, lishe na usimamizi wa rasilimali. Shabaha ya majadiliano hayo ni kutafuta suluhu ya changamoto ya upatikanaji wa chakula duniani, ambayo inachochewa na mabadiliko ya tabianchi.

Rais Dkt. Samia ni mionganini mwa Marais wanne kutoka Afrika, waliopewa heshima ya kushiriki na kuchangia kwenye mjadala huo wenye kaulimbiu isemayo: Mbegu za Fursa: Kuunganisha Vizazi na Kustawisha Diplomasia (*Seeds of Opportunity: Bridging Generations and Cultivating Diplomacy*). Viongozi wengine watakaoshiriki ni kutoka nchi za Sierra Leone, Madagascar na Nigeria.

Mbali na Mjadala huo, Rais Dkt. Samia pia atashiriki hafla ya utoaji tuzo ya **World Food Prize** kwa mwaka 2024 kwa watu wenye mchango mkubwa katika sekta ya kilimo, ikiwa ni mwendelezo wa kumuenzi Hayati Dkt. Norman E. Borlaug aliyehamasisha usalama wa chakula duniani kwa watu wote.

Sambamba na kushiriki kwenye majadiliano hayo, Rais Dkt. Samia atakutana na kufanya mazungumzo (**round tables discussion**) na viongozi kutoka Serikali na sekta binafsi ya Marekani, hususan waliopo kwenye sekta ya kilimo kwa lengo la kujadili uwekezaji katika sekta hiyo na kuongeza mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo ambayo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,
Jitokeze Kushiriki Uchaguzi



Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,
Jitokeze Kushiriki Uchaguzi